



**JAMHURI YA MUUNGANO WA
TANZANIA
WIZARA YA MAJI**



**MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA
MAZINGIRA MUSOMA**

**MKATABA WA AJIRA YA KAZI YA UJENZI WA TANGI LA MAJI LENYE
MITA ZA UJAZO 300 PAMOJA NA KUPIGA LIPU YA NDANI NA NJE YA
TANGI KATIKA KILELE CHA MLIMA KWANGWA**

KATI YA

BW. JOSEPH JAMES MWITA

NA

**MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA MUSOMA
(MUWASA)**

**MRADI WA UPANUZI WA MTANDAO WA MAJI KWENDA KATIKA MITAA SABA YA
MANISPAA YA MUSOMA ISIYOPATA HUDUMA YA MAJI**

Mkataba huu umefanyika leo tarehe 19.....Mwezi 01..... Mwaka 2022.....

Kati ya

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Musoma (MUWASA) S.L.P 233 Musoma
(ambaye katika mkataba huu anajulikana kama "Mwajiri")

Na

Bw. JOSEPH JAMES MWITA..... mwenye simu namba 0625093609
(ambaye katika mkataba huu anajulikana kama "Mwajiriwa/Fundi Uashi")

1. AINA YA MKATABA

Mkataba huu ni wa kazi maalum ya ujenzi wa tangi la maji lenye mita za ujazo 300 pamoja na kupiga lipu ya ndani na nje ya tangi katika kilele cha Mlima Kwangwa kwenye mradi wa **UPANUZI WA MTANDAO WA MAJI KWENDA KATIKA MITAA SABA YA MANISPAA YA MUSOMA ISIYOPATA HUDUMA YA MAJI**

2. KUANZA KWA MKATABA

Utekelezaji wa mkataba huu utanza mara baada ya pande zote mbili za mkataba kuweka saini.

3. ENEO LA KAZI

Kazi hii ya kujenga tangi la maji lenye mita za ujazo 300 pamoja na kupiga lipu ya ndani na nje ya tangi itafanyika katika kilele cha Mlima Kwangwa.

4. MALIGHAFI ZA UTEKELEZAJI WA KAZI MAALUM

Vifaa vyote vya kazi vitanunuliwa na Mwajiri.

5. GHARAMA YA KAZI MAALUM

Gharama za kazi zote atakazofanya Mwajiriwa ni Shilingi za Tanzania Milioni Kumi na Tano (15,000,000/=) tu.

6. UTARATIBU WA MALIPO

- a) Mwajiriwa atalipwa malipo ya awali jumla ya Shilingi za Tanzania Milioni Sita (6,000,000/=) tu.
- b) Mwajiriwa atalipwa malipo ya awamu kulingana na pendekezo la msimamizi wa mradi.
- c) Mwajiriwa atalipwa malipo yote kupitia benki. Ambapo mwajiriwa anatakiwa kupeleka akaunti namba katika ofisi ya uhasibu ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Musoma.

7. KUKOMA KWA MKATABA

Mkataba huu utafikia ukomo baada ya kazi kukamilika, kukaguliwa na kukabidhiwa kwa msimamizi wa mradi au kusitisha mkataba huu endapo mwajiri hataridhika na utendaji kazi/nidhamu ya mwajiriwa.

8. SHERIA ITAKAYOTUMIKA

Mkataba huu utaongozwa na kusimamiwa na sheria ya mikataba na sheria nyingine za Tanzania.

9. MAREKEBISHO YA MKATABA


Mwajiri na Mwajiriwa wanaweza kubadilisha baadhi ya masharti ya mkataba kwa makubaliano ya pamoja kwa njia ya maandishi.

10. KUSAINIWA KWA MKATABA

Mkataba huu umesainiwa leo tarehe...19... Mwezi...01... Mwaka 2022

Kwa Niaba ya Mwajiri:

Jina: NICAS MUGISHO
Sahihi: N. Mugisho
Cheo: Ag. M.D.



Shahidi

Jina: BURDAN KAGIRI
Sahihi: [Signature]
Cheo: Ag. TM

Mwajiriwa:

Jina: JOSEPH JAMES MWITA
Sahihi: [Signature]
Cheo: FUNDI UASHI

Shahidi

Jina: JOSEPH JAMES MWITA BOMPHAZI
Sahihi: [Signature]
Cheo: M. SAIDI